# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MOI GIRLS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MOI GIRLS SCHOOL - NAIROBI KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**

**Karatasi ya 2**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**Ufahamu.**

1. (a) Kuelimisha akina mama wazinduke ili waweze kujitegemea kiuchumi.
   (b) Kuhamasisha maendeleo ya wanawake. *al 2*
2. Waliunga mkono sera nzuri ya kusaidia wanawake.
3. Wao waliwanyanyasa wanawake kwa sababu ya ubabedume hasa katika kuwanyima wanawake fursa ya kujikimu kimaisha.
4. 
   -Wao wamepata mikopo na kuanzisha biashara zao wenyewe.
   -Wao wananunua ardhi yao sasa.
5. 
   -Imani potovu eti wanaume ndio wanastahili kuleta riziki.
   -Kutokopa fedha za kuanzisha biashara zao wenyewe.
   -Kuamini kwamba utajiri ni hifadhi ya wanaume.
6. (i) Kuwaza / kufikiria kwa makini.
   (ii) Kuwaondoa katika umaskini uliokithiri.
   (iii) Pato la kusaidia mahitaji ya kimsingi ya kila siku.

Muhtasari.

(a)
-Ili kujiondoa kutoka umaskini ni lazima tuthamini kilimo/tukipe kilimo umuhimu.
-Mamilioni ya wakenya / zaidi ya wakenyea milioni kumi wanaweza kufa njaa / kwa sababu ya njaa.
-Sababu ya njaa ni kupuuzwa kwa kilimo.
-Wakenya asilimia sabini na tano hutegemea kilimo kwa chakula na fedha.
-Kilimo hotoa nafasi za kazi.
-Huletea serekali robo ya mapato yake. *(kila hoja al. 1 x 6 = 6)*

(b)

- Serikali za Afrika na wanaopanga masuala ya uchumi kujitahidi ili kumaliza njaa na umaskini.
- Wanafunzi wakulima wa mashamba madogo kukuza na kuzalisha matunda na mboga na kufuga wanyama na ndege.
- Kuanzisha nafasi za kazi.
- Serikali kufadhili kilimo.
- Kupunguza gharama za pembejeo.
- Kuweka sera zinazodhibiti kilimo.

- Kuongeza sehemu ya bajeti ya kilimo.

- Tusipofanya hivyo tatuzidi kuomba misaada tutoka mataifa. *(al 6 - kila hoja moja 1 x 6 = al 6)*

  a - 06
  b - 06
  ut - 03

* *Makosa ya sarufi; kila kosa ilinapojitokeza,huadhibiwa kwa kuondoa $^1/_2$ alama hadi makosa 6 x $^1/_2$ = alama 3. Mtahiniwa akipata 0 makosa ya sarufi huondolewa.*

* *Makosa ya hijai/tahajia huondolewa hadi makosa 6 x $^1/_2$ = al 03*

* *Mtahiniwa akizindisha kwa maneno 10 aondolewe alama 1, baadaye akizidisha kwa 5 ondoa $^1/_2$*

* *Mwanafunzi asipotiririsha kazi yake asituzwe alama za utiririko hasa akiorodhesha hoja au aandnike vistari kabla ya hoja, atuzwe 0 katika sehemu ya utiririko.*

<u>Matumizi ya lugha.</u>

a) Sifa za sauti /h/ *al 3 x 1 = al 3*

   i) kikwamko

   ii) Sighuna / hafifu

   iii) Hutamkiwa kooni / glota *3 x 1 = al 3*

b) Dhana tatu za sentensi.

   i) Mwaura, amekuja.
   Mwaura amekuja!
   Mwaura amekuja?
   Mwaura: Amekuja.

a) Lewa - Levuka. *2 x 1 = al 2*

b) Nitakununulia kiguo na kukutembeza kijijini. Ukimaliza kijikate hicho. *2 x 1 = al 2*

c) Kuandika kwa umoja.
Walaka wangu uliwasilishwa rasmi kwako na diwani wa chama tawala. *2 x 1 = al 2*

d) Wananchi wote wanaosumbuliwa na majambazi wameletewa askari kituoni ili wawalinde.
*2 x 1 = al 2*

e) Usemi wa taarifa.
Mkulima alisema kwamba siku hiyo angechimba mtaro uelekeze maji shambani mwake.

*3 x 1 = al 3*

a) (i) Tulicheza kutoka asubuhi hadi adhuhuri (wakati)
(ii) Wezi walinikimbiza hadi nyumbani mwangu (mahali) *2 x 1 = al 2*

b) Ku - Kiambishi cha nafasi ya pili.
ni - Ndani ya
ko - Mahali.
Ki - Udogo wa nomino. *4 x $^1/_2$ = al 2*

c) (i) Mwanafunzi – kiima
(ii) Insha - Shamirisho kipozi.
(iii) Vizuri – chagizo *3 x 1 = al 3*

(k) Kukanusha kwa kutumia 'amba'
Sitavaa viatu visivyo safi. *2 x 1 = al 2*

(l) Umoja wingi

| | | |
|---|---|---|
| (i) | M - WA | Mtoto - <u>Wa</u>toto |
| (ii) | MW - WA | <u>Mw</u>alimu - <u>Wa</u>limu |
| (iii) | Ki - VI | <u>Ki</u>boroto - <u>Vi</u>roboto |
| (iv) | ch - vy | <u>Ch</u>ura - <u>Vy</u>ura |
| (v) | m - mi | <u>Mt</u>ume – <u>Mi</u>tume |

*3 x 1 = al 3*

(m) S - $S_1$ + U + $S_2$ $S_2$ - KN + KT
SI - KN + KT KN - N + V
KN - N N - wazazi
N - watoto V - wakorofi
KT - T + E KT - T + E + E
T - wanacheza T - wanawabeza
E - vizuri E - vikali
U - ilhali E – Sana *16 x $^1/_4$ = al 4*

(n) Kuainisha mofimu
A - kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja.
li - kiwakilishi cha wakati uliopita
ye - kirejeshi 'O'
m - mtendewa
let - mzizi
e – kiendelezi mnyambuliko
a – kiishio *6 x $^1/_2$ = al 3*

(o) (i) wale - kiashiria / kionyeshi - kivumishi
(ii) wale - kupata chakula - (kitenzi) *2 x 1 = al 2*

(p) **Kitenzi** **Kivumishi**

| Kitenzi | Kivumishi | |
|---|---|---|
| Dhuluma | Dhalimu | *2 x 1 = al 2* |

**<u>ISIMU JAMII</u>**

1. **<u>Ushindani kutoka lugha nyingine kama kiingereza.</u>**
   - -Hadhi - Kiswahili kimedumisha.
   - -Athari za lugha ya mama.
   - -Mitazamo hasi kuhusu Kiswahili.
   - -Kutokuwepo kwa sera mwafaka kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa muda mrefu.
   - -Kuhusishwa kwa lugha ya Kiswahili na dini ya kiislamu / eneo la pwani.
   - -Wamishenari walieneza dini zao kwa lugha ya kiingereza.
   - -Kutokouwa na vitabu vya kutosha vilivyoandikwa kwa Kiswahili.
   - -Uchache wa wataalamu wa lugha za kikabila katika shule za msingi.
   - -Kuwepo kwa sheria katika shule kuwa Kiswahili kizungumzwe siku moja kwa juma.
   - -Lugha imetengwa katika matumizi ofisini za kiserikali.

2. <u>Mikakati inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya.</u>

   -Sera madhubuti - hii itaelekeza hatua za kupanga na kuendeleza lugha. Pia itabainisha nyanja namaeneo ya matumizi ya Kiswahili.

   - Kuamrisha Kiswahili - kitumiwe kama lugha ya kufundisha baadhi ya masomo, somo la lazima n.k

   -Ufadhili wa miradi ya utafiti.

   -Maandalizi mema ya walimu na wataalamu wa Kiswahili.

   -Kubuni vyombo vya kukuza Kiswahili.

   -Kusisitiza matumizi ya lugha sanifu.

   -Serikali kufadhili uandishi na uchapishaji wa vitabu vya sarufi.

   -Kuingiza Kiswahili kwenye kompyuta.

   -Kuunda jopo la kitaifa la wataalamu - lengo lao ni kutoa mwongozo kuhusu Kiswahili.